JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Anwani ya Simu:"UCHUNGUZI"
Simu Nambari: (027) 2645186
Nukushi: (027) 2647885
Barua Pepe: rbctanga@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz

Barabara ya Hospitali ya bombo,
S.L.P 1953,
21105 TANGA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

AGOSTI, 2022

TAKUKURU TANGA YAENDELEZA USHIRIKIANO NA CHAMA CHA SKAUTI KATIKA UELIMISHAJI DHIDI YA RUSHWA

Ndugu wanahabari,

Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninawakaribisha tena katika ofisi za TAKUKURU (M) wa Tanga. Nimewaalika ndugu zangu wanahabari kama nguzo muhimu katika jamii kwa uwezo wenu wa kutuunganisha sisi kama TAKUKURU na wananchi hususani tunapotoa taarifa mbalimbali kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa. **Karibuni sana.**

Ndugu wanahabari,

Kama ulivyo utaratibu wetu, tumemaliza robo ya nne ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na tumeuanza mwaka mpya wa fedha yaani 2022/2023, hivyo nimewaita ili kuuhabarisha umma kuhusu kazi zilizofanyika katika kipindi hicho.

Ndugu wanahabari,

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007, TAKUKURU ina wajibu wa kuchukua hatua muhimu katika kuzuia na kupambana na rushwa katika jamii, Taasisi za Umma na katika Sekta Binafsi. Sisi Maafisa wa TAKUKURU tunatakiwa kufuatilia na kuchunguza shughuli na taratibu za jamii, Taasisi za Umma na Binafsi, ili kuwezesha kufanya ugunduzi wa

Kutokana na matokeo hayo TAKUKURU Mkoa wa Tanga ilipendekeza Taasisi zinazotumia huduma za TEMESA zijitahidi kulipa madeni yao kwa wakati ili kuipa uwezo TEMESA wa kufanya kazi zake kwa kujiamini na kuwapunguzia madeni kwenye maduka ya vifaa. Lakini pia tulishauri kuwa TEMESA ipunguze madeni wanayodaiwa na maduka ya vifaa vya magari ili waweze kuaminiwa na kupata huduma kwa bei nzuri.

Pamoja na madeni hayo kulipwa TAKUKURU Mkoa wa Tanga imeshauri Serikali iboreshe huduma za TEMESA kwa kuipa uwezo wa kuwa na stoo yenye spare za kutosha kuliko kutegemea kununua madukani ili kuweza kupunguza malalamiko ya gharama kubwa za vifaa. Serikali iongeze Rasilimali watu na vitendea kazi ili kurahisisha utendaji kazi wa TEMESA.

Aidha zimefanyika **warsha 09** ambapo TAKUKURU Mkoa wa Tanga imekaa na wadau husika na kujadili matokeo ya chambuzi zilizofanyika na kuwekeana mikakati ili kuondoa mapungufu yaliyobainika pamoja na mianya ya rushwa. Baadhi ya maazimio yaliyowekwa katika warsha ya TEMESA ni kuwa wateja wa TEMESA waendelee kutumia huduma za TEMESA hususani kwenye matengenezo ya magari lakini TEMESA itawepeleka mafundi wake kwenye kozi ndogo ndogo ili kuondoa tatizo la Mafundi kutokuwa na ujuzi hasa kwenye matengenezo ya magari ya kisasa; Jambo linguine ni kuanzisha karakana shirikishi wilayani hasa katika wilaya zilizoko mbali na ofisi za TEMESA na pia madeni yapunguzwe kwa Taasisi zinazodaiwa.

Ndugu waandishi wa Habari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga sio tu kuwa tunafanya uchambuzi wa mifumo, kufanya warsha na kuweka maazimio peke yake, bali tunafanya pia ufuatiliaji ili kujiridhisha iwapo maazimio tuliyoyaweka yanatekelezwa ipasavyo. Kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2022 jumla ya maazimio yaliyowekwa kutokana na warsha 6 yamefuatiliwa na kubaini kuwa utekelezaji wa maazimio unaendelea.

Ndugu wanahabari,

Kifungu cha 7 (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007, kinaitaka TAKUKURU kuhimiza na kuendeleza uungwaji mkono wa jamii katika kupambana na vitendo vya Rushwa. Sisi tunatekeleza jukumu hili kwa kuelimisha na kushirikisha wadau na umma kwa ujumla katika mapambano dhidi ya rushwa.

ulishafanyika na taarifa zimewasilishwa kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kama alivyoagiza.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Tanga imejiwekea utaratibu wa kuwafikia wananchi kwa njia ya kampeni ya **TAKUKURU INAYOTEMBEA**. Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022, tumewafikia Watumishi na Watumiajii wa Bandari ya Pangani na kuwapa Elimu Juu ya Rushwa na Athari zake na kisha kuzungumza nao kuhusu kero za huduma mbalimbali katika Bandari hiyo.

Wananchi hao walishiriki semina kwa ari na mambo ambayo waliyaibua na yanayohitaji maboresho ni pamoja na suala la Usalama.

- Kwamba alama za usalama bandarini hapo hususani alama za maingilio ya vyombo vya majini hazionekani
- Kwamba miundombinu na vyombo vya uokoaji ni hafifu kiasi cha kupelekea watumiaji wa bandari kuwa na wasiwasi wa usalama wao iwapo ikitokea ajali au dharula yoyote.
- Aidha wananchi hao walizikumbusha mamlaka husika kuzingatia usalama kwa kuweka alama zinazowaongoza watumiajii wa bandari pamoja na kuimarisha miundombinu ya ukoaji.

Tuliweza pia kuwafikia Vijana wa Kituo cha Bodaboda cha Kivukoni Wilayani Pangani na kuwapa Elimu ya Mapambano dhidi ya rushwa

Ndugu wanahabari,

UCHUNGUZI NA MASHTAKA:

Katika jukumu la kuchunguza tuhuma au makosa ya Rushwa pamoja na njama za kutendeka kwa makosa hayo, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imepokea Jumla ya Taarifa **140** na kati ya taarifa hizo, **72** ni za vitendo vya rushwa na taarifa **68** si taarifa za vitendo vya rushwa.

Taarifa **72** zilizohusu Rushwa zilifunguliwa majalada ya uchunguzi ambapo taarifa **31** zinaendelea kuchunguzwa na taarifa **41** zimefungwa kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha tuhuma.

Rushwa Namba 11/2007. Kifungu hiki kinatamka wazi kwamba kila mtu ambaye ana taarifa juu ya mtu kutenda kosa au kusudio la mtu kutenda kosa chini ya sheria hii, awe anafahamu kabla au baada ya kosa kutendwa, anatakiwa kutoa taarifa TAKUKURU.

Tafadhali ninawasihi sana, yeyote mwenye taarifa inayohusu vitendo vya rushwa afike ofisi yetu ya mkoa iliyopo BOMBO AREA karibu na HARBOURS CLUB na kwa wale waishio wilayani wasisite kufika katika ofisi za TAKUKURU zilizopo katika Wilaya husika. Ninaomba niwasihi pia kuitika wito wa Mahakama pale mtakapohitajika Kutoa ushahidi mahakamani ili kwa pamoja tukamilishe mchakato wa haki jinai katika Mapambano dhidi ya rushwa.

Unaweza kutumia Huduma ya BURE kwa kutupigia simu ya dharura namba 113 au kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kisha kufuata maelekezo, ili kututaarifu juu mtu yeyote anayekiuka sheria na kufanya uhalifu kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Wahenga walipata kunena kwamba kidole kimoja hakivunji chawa na pia Umoja ni nguvu. Hivyo, Kumbukeni kuwa hii vita ni yetu wote na kwa umoja wetu, kuishinda rushwa na kuifikia Tanzania isiyokuwa na Rushwa, **INAWEZEKANA.**

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Imetolewa na:

Nestory Gatahwa
K.n.y: MKUU WA TAKUKURU (M)
TANGA
Simu 0738 – 150225

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022